

SAADUN OMAR TAMBWE

- S** Sasa ngoja nikwambie, maneno ninayotaka,
Soma uyazingatie, kama hayana mashaka,
Si kitu uyaachie, kama mithili ya taka,
Sitiri unae taka, kwani sudi iko kwako.
- A** Ama kweli ujijue, bahati inakutaka,
Au sivyo utambue, hapo kaka singefika,
Aidha ungechelee, au jambo kujitwika,
Ahidi kutukumbuka, kwani sudi iko kwako.
- A** Akhi usimuachie, aende akizunguka,
Ambapo wewe mwenzie, wapata hadi wachoka,
Akibayo mtolee, shida aende inyuka,
Acha kubania kaka, kwani sudi iko kwako.
- D** Daima usiachie, pia sala kuzishika,
Dhambi uziangalie, huku ukikasirika,
Dini yako uijue, na kutenda innotaka,
Deni liondoe kaka, kwani sudi iko kwako.
- U** Ukae na utulie, heshima iwe kwa kaka,
Utashi ujitendee, kwa ushauri wa kaka,
Ungana nao wazee, ikiwa kwako tafika,
Uache akhi zunguka, kwani sudi iko kwako.
- N** Naona hapa nishie, mengi hayo nimetwika,
Nena neno jinenee, kama haya taka taka,
Nadi mazuri na wewe, mtima kuupulika,
Nema kwako zitafika, kwani sudi iko kwako.

Hamidu Rajabu Tambwe
MBEYA, Tanzania. 04/04/1968
